# Learning by Ear – Girls' Rights

**Episode 04**

**Title: Inheritance - A story of Girls' Rights**

**Author: Njoki C. Muhoho**

**Editors: Andrea Schmidt, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Michael Lawton**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters:**

**SCENE 1 MAMA CIRO'S HOMESTEAD**

Narrator - Male - 30s
Cheptoo - Female - 15 years
Ciro – Female - 15 years
Fatuma - Female - 14 years

**SCENE 2 MAMA CIRO'S COMPOUND ELDERS' MEETING**

Uncle Babu - Male – 60s
Mama Ciro - Female - 40s
Ciro – Female - 15 years
Narrator - Male - 30s
4 elders – Male and Female – 50-70 years

**SCENE 3 SCHOOL PLAY FIELDS**

Ciro – Female - 15 years
Fatuma - Female - 14 years
Cheptoo - Female - 15 years
Narrator - Male - 30s

**SCENE 4 GIRLS' PARLIAMENT ON THE PLAYING FIELDS**

Cheptoo - Female - 15 years
Fatuma - Female - 14 years
Abdi - Male - 16 years
Narrator - Male - 30s
Group of students (parliament)

**SCENE 5 GATHERING WITH TEACHER MONA – CLASSROOM**

Teacher Mona - Female - 35 years
Fatuma - Female - 14 years
Cheptoo - Female - 15 years
Abdi - Male - 16 years
Janet Social worker - 30s
3 Boys
2 Girls (including Ciro)
Narrator - Male - 30s

**INTRO**

**01. MUSIC: THEME MUSIC**

02. **NARRATOR** Hujambo na karibu kwa Makala ya nne kwenye mfululizo wa vipindi vya Learning By Ears Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu '**Haki za Wasichana'.** Katika kipidindi kilichotangulia, Marafiki watatu Ciro, Cheptoo na Fatuma waelimishwa kuhusu visa vya unyanyasaji wa Kimapenzi na jinsi ya kuzuia visa hivi.Wasichana nao wanaonywa dhidi ya kuvichukulia visa kimzaha kwamba ni mapenzi ya kawaida ya wavulana.
Na leo katika makala hii, tunasikia jinsi wasichana wanavyojadilia hoja kuhusu masuala ya urathi. Endelea kuwa nasi.

**SCENE 1: MAMA CIRO HOMESTEAD**

**03. SFX: FARM NOISES**

**04. SFX: CIRO IS CRYING**

05. **CHEPTOO** (COMFORTING) CIRO,Tafadhali usilie. Jipe moyo!.

06. **CIRO** (CRYING) Ni uchungu. Babangu ameniacha!. Ameniacha !

07. **FATUMA** CIRO Jikaze. Tuko hapa na wewe kukufariji. Marafiki wako wote, Cheptoo pia yuko hapa….!

08. **CHEPTOO** .. hata Fatuma yuko hapa.Tumekuja kukufariji. Usilie CIRO.

09. **CIRO** (CRYING) Wakati mwingi amekuwa akiishi mjini, mabli na mimi na sasa ameniacha. Kumuachia Ba-Mdogo Babu jukumu la kunilea.

10. **CHEPTOO** Babako mdogo Babu yuko atamsaidia mamako. Kwani mamako yuko wapi?

11. **CIRO** Yuko pale na wazee. Wako kule nje wakipanga kuhusu maisha yetu ya baadaye.

12. **FATUMA** Twendeni tusikilize ni mipango gani wanayojadilia.

**SCENE 2 : MAMA CIRO'S COMPOUND ELDERS MEETING**

**13. SFX: ELDERS MURMURS INCREASE (studio)**

| | | |
|---|---|---|
| 14. | **UNCLE BABU** | Tusikilizane tafadhali, tusikilizane. Ni huzuni kumpoteza Kakangu mkubwa. Mungu alilaze roho yake mahali pema peponi |
| 15. | **ALL** | Ameeeen. |
| 16. | **UNCLE BABU** | Lakini maisha lazima yaendelee.Tuone jinsi ya kuwasaidia walioachwa nyuma. Mama CIRO na CIRO ni Wanawake katika familia hii. Jukumu letu ni kuhakikisha kuwa tunawashughulikia kadri ya mapenzi ya marehemu Kakangu. |
| 17. | **MAMA CIRO** | (SNIFFLING) ooh ametuacha mapema. Tunamshukuru maana ametuachia shamba na nyumba. |
| 18. | **UNCLE BABU** | CIRO, njoo hapa. Unapasa kufahamu sisi wazee tunakupangia nini katika siku zako za usoni. Uko wapi wewe msichana. Njoo hapa karibu!. |
| 19. | **CIRO** | Niko hapa Ba-mdogo. |

20. **UNCLE BABU** CIRO, na Mama CIRO, Sitaki muwe na hofu kuhusu maisha yenu ya baadaye. Mimi kama Kaka mkubwa wa marehemu Baba Ciro, Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi , nitafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba munaishi vizuri.

21. **MAMA CIRO** (SNIFFLING) Asante sana. Mimi na Ciro tunafurahi kwamba tuko na wewe. Umetushughulikia wakati marehemu mume wangu alikuwa hayuko karibu akifanya kazi mjini.T(CRYING)Siamini ametuacha mapema hivi!.

22. **UNCLE BABU** Usilie Mama CIRO. Niko hapa kumshughulikia. Kuanzia kesho, nitaanza kusimamia shamba hili. Wewe na Ciro mtakuja kuishi na mimi kwangu nyumbani.

23. **CIRO** (ALARMED)Tuhamie kwako? kwanini? Hapana..hapa ndio nyumbani kwetu!.

24. **UNCLE BABU** Wewe msichana, huyaelewi mambo haya. Unahitaji Mwanamume kama ngao kuwatunza nyinyi,shamba na hata nyumba yenu pia. Mimi nitasimamia shamba na nyumba hii.

| | | |
|---|---|---|
| 25. | **MAMA CIRO** | Mzee Babu, nafahamu vyema tamaduni zetu, lakini naomba mutuache mimi na binti yangu tuishi kwa nyumba hii yetu. |
| 26. | **UNCLE BABU** | Kulingana na mila na tamaduni zetu, kuanzia leo, mali yote ya marehemu kakangu iko mikononi mwangu.Hizo ni sheria za urathi katika mila na tamaduni zetu. Mama CIRO na Ciro kama wanawake wa nyumba hii, pia mtakuwa chini ya urithi wangu. |
| 27. | **CIRO** | (ALARMED) Baba Mdogo huwezi kuturidhi. Sisi tutaishi hapa katika nyumba hii na tutaendelea kusimamia shamba letu. |
| 28. | **UNCLE BABU** | (ANGRY) Wewe ni msichana mdogo, hufahamu chochote kuhusu utamaduni wetu. Mimi kama babako mdogo, nitarithi mali ya marehemu Kakangu. Pamoja na mwanangu Abdi, tutashughulikia mahitaji yenu yote. |
| 29. | **CIRO** | Mimi na mamangu tuuwezo wa kushughulikia mahitaji yetu wenyewe. |

30. **NARRATOR** Ni jambo linalomshangaza Ciro baada ya kufahamu kwamba yeye na Mamake hawawezi kurithi mali ya marehemu babake. Mali yote inarithiwa na Wanaume katika jamii hiyo.

Je rafiki za Ciro, Fatuma na Cheptoo watalichukulia vipi suala hili?

**<u>SCENE 3 SCHOOL PLAY FIELDS</u>**

**31. <u>SFX: PLAY FIELD NOISES</u>**

32. **CIRO** (CRYING) Nimechanganyikiwa Fatuma!. Sasa mimi na Mamangu tutaishi wapi?

33. **FATUMA** CIRO pole sana kwa kumpoteza Babako!. Mimi na Cheptoo tutakusaidia kadri ya uwezo wetu.

34. **CHEPTOO** Wewe na Mama yako msikubali kuondoka katika nyumba hili lenu. Na hofia kwamba Babako mdogo anaweza hata kumuoa Mamako kuwa Mke wa nne.

35. **FATUMA** ssssh.Cheptoo, Usije kuyafanya makubwa zaidi mambo haya. Sasa tufanyeje?

36. **CHEPTOO** Tuitishe kikao cha bunge. Namuona Abdi akija . Pia yeye tutamualike pamoja marafiki wake wote.

37. **NARRATOR** Na kama ilivyo kawaida sasa, wasichana hawa wanaitisha kikao cha bunge lao wanapokuwa na hali kama hii ya utata. Na wakati huu wanawaalika marafiki wachache kwenye kikao cha dharura katika uwanja wa kichezo.

Ufumbuzi wa tatizo hili bado ni kitendawili na ndio maana wanataka kusikia maoni kutoka kwa wengine.

**SCENE 4 AT PARLIAMENT ON THE PLAYING FIELDS**

38. **SFX: MUMURS OF STUDENTS**

| | |
|---|---|
| 39. **CHEPTOO** | Tusikilizane, hatuna muda mwingi.. ni dakika chache tu za kujadiliana!.Kama mjuavyo Ciro amempoteza Babake. Na sasa Babake mdogo anatishia kuchukua shamba na Nyumba yao pia …eti kwa kisingizio cha utamaduni.<br><br>Tumemuallika nyinyi wavulana ili tuweze kulijadilia suala hili kwa pamoja.<br><br>Napendekeza hoja, kwamba Ciro na Mamake waendelee kuishi katika nyumba yao na kujishughulikia wao wenyewe. |
| 40. **FATUMA** | Kwa niaba ya wasichana wote hapa, naunga mkono hoja hiyo. |
| 41. **ABDI** | Na mimi kwa niaba ya wavulana wote hapa napinga hoja hiyo. |
| 42. **CHEPTOO** | Sasa mjadala uko wazi.Fatuma? |
| 43. **FATUMA** | CIRO anahitaji kuishi katika nyumba yake alikozaliwa. |
| 44. **ABDI** | Si nyumba yake. Yeye ni msichana. Ni nyumba ya Babake. |

| | | |
|---|---|---|
| 45. | **CHEPTOO** | Yeye na nyumba hiyo ni kitu kimoja. Anahaki…! Pia mamake anahaki ya kumiliki nyumba hiyo!. |
| 46. | **ABDI** | CIRO ni mtoto, lazima amheshimu Babangu ambaye ni Babake mdogo. |
| 47. | **FATUMA** | Jukumu lake kubwa ni kumshughulikia Mamake. |
| 48. | **ABDI** | Wanawake hawana haki ya kurithi mali.! |
| 49. | **CHEPTOO** | Nani kasema hivyo? Mamake amekuwa akilima katika shamba hilo na kutunza familia yake miaka nenda miaka rudi,kisha ghafla anakuwa hana haki. |
| 50. | **ABDI** | Lakini hana hata kuku katika shamba hilo. Sasa kila kitu kilichomo ndani ni mali ya Babangu. Amerithi. |
| 51. | **CHEPTOO** | (UPSET) Abdi, unafahamu uanchosema? CIRO na mamake ni Binadamu kama wengine. Wana haki! |
| 52. | **ABDI** | Haki ya kutunzwa….! |
| 53. | **CHEPTOO** | Kutunzwa! Hawahitaji msaada wowote. |
| 54. | **ABDI** | Lakini ni wanawake!. |

| | | |
|---|---|---|
| 55. | **CHEPTOO** | (ANGRY) Usinikasirishe!! Wewe ni mjinga sana..!. |
| 56. | **FATUMA** | Punguza hasira Cheptoo..! Nyinyi wawili punguzeni hasira!. |
| 57. | **ABDI** | Ndilo tatizo kubwa la wasichana. Hamsikizi. Niwadhaifu sana, na mnahitaji kutunzwa, Nyinyi ni wazuzu hamujielewi.. |

**58. <u>SFX: SCUFFLE (studio)</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 59. | **CHEPTOO** | (ABDI) Wewe…wewe... wewe ndie mjinga, nyinyi wavulana mnjifanya mnajua kila kitu na haki ya umiliki.. Mimi …nita… |

**60. <u>SFX: SCUFFLE</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 61. | **FATUMA** | (ALARMED) Nyamazeni sasa |

**62. <u>SFX: LOUD CRYING BY CIRO (studio)</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 63. | **FATUMA** | Sasa waona ulivyofanya!.Tuko hapa kumsaidia Ciro na sasa unamuongezea machungu kumfanya alie hata zaidi. |

**64. <u>SFX: CRYING CONTINUES</u>**

65. **CHEPTOO** (APOLOGETIC) Pole Ciro, nilikuwa najaribu kukutetea….Si kukusudia kukuzidishia majonzi.

**66. SFX: CRYING CONTINUES**

67. **ABDI** Sawa waona, nyinyi wasichana hamuwezi kusimamia mali. Mna hasira za haraka sana.

**68. SFX: SCHOOL BELL RINGS**

69. **FATUMA** CIRO, hebu turudi darasani.Tunahitaji ushauri kutoka kwa Mwalimu Mona. Njoo twende, walimu anatusubiri.

70. **NARRATOR** Mambo hayakwenda kama ilivyotarajiwa.Nani mkweli na nani muongo? Hakuna ajuaye. Habu tumsikilize Mwalimu Mona ambaye anawapa muongozo katika suala hili muhimu.Endelea kusikiliza…

**SCENE 5: GATHERING WITH TEACHER MONA – THE PARLIAMENT**

71. **TEACHER MONA**

Wasichana na wavulana, kwanza,tunataka kutoa pole zetu kwa rafiki yetu Ciro. Kama mjuavyo amempoteza Babake.Hivyo Tukao kimywa kwa dakika moja kutoa heshima zetu kwa marehemu Baba Ciro.

**SILENCE**

72. **TEACHER MONA**

Kikao cha bunge la Wasichana sasa kimeitishwa kujadili hoja kuhusu urathi kwa wanawake. Ciro na Mamake wanakumbwa na tisho la kupoteza mali yao kwa Wanaume katika familia yao.

Nimemualika Afisa wa masuala ya jamii Bi Janet naye achangie kidogo katika hoja hii.

Fatuma, umetuita hapa, sasa twambia hoja yako tafadhali.

(FIRMLY) Kwanza yatupasa kila mmoja wetu aonyeshe moyo wa huruma kwa Ciro hasa katika kipindi hiki kigumu cha maombolezi.Pili ningemuomba kila mmoja ajaribu kujizuia hasira zake. Fatuma?

| | | |
|---|---|---|
| 73. | **FATUMA** | Hoja yetu leo ni, 'Je Wanawanake na wasichana waruhusiwe kurithi au kusimamia mali' za Baba na waume zao?. |
| 74. | **TEACHER MONA** | Wanaopinga hoja hiyo.., Abdi, unaweza kutueleza msimamo wako? |
| 75. | **ABDI** | Wanawake na wasichana hawapasi kurithi Mali. Ni kikumu la Wanaume katika familia kurithi au kusimamia mali zote ikiwa ni pamoja na kuwatunza Wanawake na wasichana katika jamii. |
| **76.** | **<u>SFX: GIRLS SNEERING</u>** | |
| 77. | **TEACHER MONA** | Order, order. Hebu tulijadilie suala hili kimantiki. Cheptoo…! |
| 78. | **CHEPTOO** | Ni dhahiri kwamba Wanawake na wasichana wana haki sawa katika suala hili. Wote wanahaki ya kumiliki au kusimamia mali. |
| 79. | **ABDI** | Kinamama na wasichana ni walezi tu. Ni walezi wa familia. Na wanapasa kuwaachia wanaume jukumu la kusimamia mali. |

| | | |
|---|---|---|
| 80. | **FATUMA** | Kwani ni nini wavulana wanacho ambacho wasichana wamekosa? |
| 81. | **ABDI** | Tunauwezo wa kusimamia kila kitu, kufanya maamuzi mbali na uwezo wa kusimamia vyema masuala ya fedha. |
| 82. | **CHEPTOO** | Samahani, mwanamazingira mashushuhuri Profesa Wangari Mathaai ni Mwanamke,Rais wa Liberia ni Mwanamke, na kuao wengine wanaosimamia taasisi kubwa kubwa za kifedha, mawaziri wa Fedha, wafanyi biashara na kadhalika. |
| 83. | **ABDI** | (STUTTERS) Sawa… Sawa |
| 84. | **CHEPTOO** | (SNEERING) Sawa nini? Sema, sema.. sawa nini? |
| 85. | **TEACHER MONA** | Order.. order…Hebu tusikie ushauri kutoka kwa afisa wa Jamii Bi Janet |

86. **JANET** Asanteni sana. Kwanza, hii ni karne ya 21, na sio zile enzi za mababu zetu. Siku hizi wanawake wameelimika iwe rasmi au kinyume. Pia wanaufahamu na wala sio kama wale Wake wa wawawindaji zamani hizo ambao walikuwa wakibakia majumbani tu wakati waume hao wanapokwenda msituni mawindoni.

87. **GIRLS** Waambie ….waambie ..

88. **JANET** Lakini haya si mashindano.Wanaume na wavulana wamekuzwa na kasumba kwamba wao ndio warithi na wanapasa kuchukua jukumu la kuwatunza Kina mama na Binti zao.

89. **BOYS** Wambie wambie ..sikizeni..

90. **JANET** Lakini katika dunia ya sasa mambo yamebadilika. Sheria zimebadilika na bado zinaendelea kubadilika.Hivi sasa katika jamii nyingi Kinamama ndio wenye haki ya kurithi mali.

91. **CHEPTOO** Hapo sasa…waambie…Wambie Bi Janet.

| | | |
|---|---|---|
| 92. | **JANET** | Cheptoo, ingawa huu ni mjadala na katika mjadala wowote lazima kuwa na mshindi. Lakini hapa hatutafuti mshindi. Ni suala la sisi kubadilisha tabia na mienendo yetu na kukumbatia suala la usawa wa kijinsia. |
| 93. | **TEACHER MONA** | Mumesikia. Sasa mnafahamu kwamba urathi ni kwa wote wavulana na wasichana bila ya kubagua. Mimi na Afisa wetu wa jamii Bi Janet tutaandamana hadi nyumbani kwa kina Ciro kukutana na wazee ili kujadilia zaidi hoja hii. Fatuma, sasa unaweza kufunga mjadala |
| 94. | **FATUMA** | Katika hoja hii ya iwapo Kinamama na wasichana wana haki ya kurithi mali, jibu ni NDIO.Lakini sote tunajukumu la kuwahamasisha Watu wetu. Mjadala huu sasa umefungwa! |

95. **OUTRO**

96. **NARRATOR**

Na hadi hapo tunafika mwisho wa kipindi cha leo cha Noa bongo jenga maisha yako kuhusu Wasichana wanaopinga tamaduni zinazowakandamiza.Katika kipindi hiki tumesikia kwamba wana haki za kurithi.Ungana nasi tena kwa kipindi kijacho cha Noa Bongo usikie ni hoja gani zitkazowasilishwa katika bunge hili la wasichana.

Endapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki au kutuma maoni, tembelea mtandandao wetu wa WWW.DW-WORLD.DE/LBE. hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.